**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**BUNGE LA KUMI NA MOJA**

**MKUTANO WA KWANZA**

**Kikao cha Tatu – Terehe 19 Novemba, 2015**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao cha Tatu cha Mkutano wetu wa Kwanza. Kama nilivyowaomba jana, natumaini kila mmoja amepitia *Order Paper.* Kwa hiyo, tunaelewa masuala yanayohusu utaratibu wa leo, siku muhimu sana Kitaifa.

Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH - KATIBU WA BUNGE:** Kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu!

**KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyokwishatusomea Katibu, shughuli yetu ya kwanza ni kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hapa nilipo bado hata mimi hilo jina sina, sijalipata. Bado ni siri kubwa! Kwa hiyo, tuwe na uvumilivu kidogo. Nina hakika nitaletewa hapa hapa. Nikikabidhiwa hapa hilo jina na kwa kuwa ni mmoja wenu anayekuwa Waziri Mkuu, basi tutaendelea na utaratibu kadiri ulivyopangwa.

Basi, ngoja nikae nisubiri subiri kidogo hapa dakika mbili tatu, nione kama hili jina nalipata sasa hivi.

*(Waheshimiwa Wabunge walitulia Ukumbini kusubiri jina la Waziri Mkuu)*

## KUHUSU UTARATIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu, ni kwamba nitakapolipata hili jina, nitaifungua bahasha mbele yenu kuwathibitishia kwamba sikuwanayo kabla. Nitalisoma lile jina kadiri tulivyoletewa na Mheshimiwa Rais. Sasa kiutaratibu inatakiwa nikishalisoma lile jina Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe hoja humu Bungeni ya kutuomba tuthibitishe.

Sasa katika kutoa hoja, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatakiwa pamoja na mambo mengine, awe na wasifu wa aliyeteuliwa. Si ndiyo jamani! Amwelezee kidogo yule aliyeteuliwa. Sasa naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale alipokaa, hana hilo jina. Kwa hiyo, nikishalitaja lile jina, itabidi tu-*break* kidogo kama muda wa saa moja ili tumpe nafasi akatengeneze maelezo kidogo ya kuja kutoa mbele ya Waheshimiwa Wabunge.

Natumaini tumeelewana katika hilo. Kwa hiyo, baada ya muda si mrefu tuta-*break* na baada ya muda, tutarudi tena hapa.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kusubiri jina la Waziri Mkuu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inabidi nimtume Katibu wangu aende akalitafute jina. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Katibu wa Bunge (Dkt. Thomas Kashililah) na Naibu Katibu wa Bunge (Ndg. John N. Joel) Walikwenda Kutafuta Jina la Waziri Mkuu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, likipatikana, kama nilivyowaeleza, litaingizwa humu ndani na mmoja wa Askari wa Bunge, akisindikizwa na Mpambe wa Bunge. Litaingizwa hapa ninyi wote mkishuhudia, nami nitalipokea hapa mbele yenu. Hiyo shughuli ni pevu kweli kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Huo ndio utaratibu wa Awamu ya Tano. Hakuna jambo ku-*leak,* "Hapa Kazi Tu". *(Kicheko/Makofi)*

Wengine walikuwa wanafikiri kwamba, dakika zile ambazo tuta-*break* ni nyingi kidogo! Niwahakikishie kwamba siyo nyingi sana kwa sababu kama nilivyosema tutampa muda Mwanasheria Mkuu kutengeneza hoja yake, lakini pia Katibu wa Bunge hangeweza kutengeneza *Ballot Paper,* ile karatasi ya kura wakati hana jina.

Nafikiri tunaelewana Waheshimiwa, eeh?

Kwa hiyo, tukishalipata jina, tuta-*break* kwa muda mfupi ili vilevile Katibu aweze kukimbia mara moja atengeneze karatasi za kura zinazoendana na jina ambalo tutakuwa tumeletewa. Ndio sababu ya mapumziko ya muda mfupi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Ndio kaka!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7). Kwa kuwa, inaonekana Serikali haijajipanga vizuri na kwa kuwa huu ni mhimili unaojitegemea; na kitendo hiki cha kutukalisha Wabunge tukisubiri Serikali ambayo haijajipanga ni kuudhalilisha mhimili mwingine wa Taifa, ni kwa nini usiahirishe Bunge mpaka hapo Serikali itakapojipanga ili tufanye mambo mengine, badala ya kukaa hapa tunaonekana kama hatuna kazi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, sisi wote tunajua kwamba Waziri Mkuu akishateuliwa na Mheshimiwa Rais anathibitishwa na Wabunge wenyewe. Kwa hiyo, hoja hii ya Mheshimiwa Mbunge anachosema, kwamba kusubiri jina ni kulidhalilisha Bunge, ni kwamba, huko siyo kulidhalilisha Bunge, isipokuwa yeye kwa kitendo chake anachokipendekeza ndicho kinachoweza kuwa kinadhalilisha Bunge, kwa sababu anataka kulifanya Bunge liache kutekeleza jukumu lake la Kikatiba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya sisi kutokujua jina mpaka sasa hivi, ni kielelezo cha dhati kabisa kwamba Serikali hii imekusudia kutunza siri zake, siyo vitu vya kuvujavuja kama ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba Wabunge tuwe na subira. Hiki ni kielelezo kizuri kabisa cha utendaji kazi kinachozingatia maadili ya Utumishi wa Umma wa kutunza siri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Msigwa kwa changamoto. Nakushukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, nawahakikishia kabisa kwamba jambo hili liko katika mikono salama. Ni kwamba jina safari hii litaingia kwa *style* tofauti na ile miaka mingine ambayo tumezoea. *Style* ambayo litaingia nayo ndio hii, baada ya muda siyo mrefu jina hilo litaingia hapa. Nimeagiza, nisiletewe karatasi

inapepeapepea, niletewe iko ndani ya *briefcase*. Liwe limefungwa mle ndani. Siri kabisa mpaka hapa, *briefcase* ifunguliwe, nikabidhiwe bahasha. *(Kicheko)*

Kwa kuwa, ni mmoja wenu anayekuwa ndio jina lake limo humo, kwa vile Katiba inasema Waziri Mkuu lazima awe Mbunge tena wa kuchaguliwa, kwa hiyo, tutulie hatuwezi kujua. Inawezekana ni mmoja wenu katika ninyi ambao mko hapa. Tutulie kidogo, mambo yanaiva sasa hivi tu. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kusubiri jina la Waziri Mkuu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshapata taarifa kwamba, jina hilo liko mitaa hii hii, karibu sasa linafika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kusoma *Order Paper. (Kicheko)*

Pia, niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, baada ya zoezi la uteuzi wa Waziri Mkuu kukamilika hapa Bungeni, tutaendelea na ratiba yetu kama ilivyo, ambapo tutakuwa na suala la Uchaguzi wa Naibu Spika na tukishampata Naibu Spika, tutahakikisha Kiapo cha Naibu Spika pia kinafanyika hapa hapa. Kwa hiyo, tuna kazi nyingi nzito za kufanya leo za kupata viongozi muhimu sana watakaotusaidia kazi, hasa katika jengo hili. Tuendelee kuwa na subira kidogo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, labda nichukue dakika hizi chache kuwapitisha kwenye utaratibu mzima kwa mara nyingine tena, ili tuwe tuna uelewa wa pamoja kuhusiana na Utaratibu wa Kumthibitisha Waziri Mkuu.

Utaratibu wa Kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu kwa kawaida unazingatia Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambapo katika Ibara hiyo inaeleza kwamba:-

*"Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile ndani ya siku kumi na nne, baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua Mbunge wa Kuchaguliwa kutoka katika Jimbo la Uchaguzi anayetokana na Chama cha Siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au, kama hakuna Chama cha Siasa chenye Wabunge wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi." (Makofi)*

Ili kutekeleza sharti hilo, Kanuni za Bunge, Kanuni ya 25(1) na (2) zinaeleza kwamba:-

"(1) Baada ya shughuli ya kuapisha Waheshimiwa Wabunge kukamilika, Spika atasoma Taarifa ya Rais inayotaja jina la Mbunge anayempendekeza kuwa Waziri Mkuu ili aweze kuthibitishwa na Bunge. *(Makofi)*

(2) Baada ya Spika, kutaja jina la Mbunge anayependekezwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi wa Mbunge husika kuwa Waziri Mkuu.

Utaratibu wa Kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu utafuata hatua zifuatazo:-

Hatua ya kwanza, Mheshimiwa Spika, ataanza kwa kutoa taarifa kuwa amepokea bahasha ikiwa imefungwa kutoka kwa Mheshimiwa Rais yenye barua inayoliomba Bunge kuthibitisha jina la Mbunge anayependekezwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bahasha yenye barua hiyo itafunguliwa kwa mara ya kwanza mbele ya Wabunge wote waliopo Bungeni na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ataifungua bahasha na kuisoma barua yenye jina la Mbunge anayependekezwa. Baada ya hapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa Hoja ya Kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha Azimio la Bunge ambalo litatakiwa kuungwa mkono na baadhi ya Wabunge.

Baada ya Hoja iliyotolewa kuungwa mkono, Katibu wa Bunge atapewa fursa ya kutoa maelezo ya utaratibu wa kuthibitisha uteuzi. Baada ya kupiga kura, zoezi la kuhesabu litafanywa na Watumishi wa Bunge walioandaliwa kwa ajili ya shughuli hiyo chini ya usimamizi wa Mawakala watakaoteuliwa na Mheshimiwa Spika.

Baada ya kura zote kuhesabiwa, Katibu wa Bunge atatoa Taarifa kwa Wabunge kuhusu matokeo ya kura zote zilizopigwa kama ilivyo kawaida ya chaguzi zetu.

Matokeo ya kura zilizopigwa yataonesha kuwa Bunge limethibitisha au limekataa kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu. Iwapo Bunge limethibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, anaweza kumwomba Waziri Mkuu Mteule kutoa neno la shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo utakuwa mzunguko wa hii shughuli yetu. Kwa kuwa, Katibu wangu amerudi sasa, ngoja nimsikilize.

*(Hapa Katibu alikuwa akimpa Taarifa Mheshimiwa Spika)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu ananitaarifu kwamba, mambo yote sasa ni tayari yameiva na bahasha hiyo, naletewa na Mpambe wa Rais mwenyewe, *ADC* wake. Kwa hiyo, sasa kwa vile ni Askari, anaruhusiwa kuingia katika Ukumbi.

Kwa hiyo, naomba *Sergeant-At- Arms* na Mpambe wa Rais, mnaruhusiwa kuingia sasa katika Ukumbi. Karibuni sana. *(Makofi)*

*(Mpambe wa Rais akisindikizwa na Sergent-At-Arm aliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mnaiona bahasha yenyewe! Iko *sealed* kabisa, kabisa!

*(Spika alionesha bahasha kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Sasa nimruhusu mgeni wetu aweze kutoka. *(Makofi)*

*(Hapa Mpambe wa Rais Aliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Nawathibitishia kabisa kwamba bahasha hii imefungwa na *seal* kabisa. Sasa nami kwa sababu nina Katibu hapa, namwomba Katibu wangu wa Bunge aje hapa afanye kazi ya Ukatibu, anisaidie tuthibitishe kabisa kwamba kweli imetoka kule kule! *(Kicheko)*

*(Hapa Katibu Alifungua Bahasha yenye jina la Waziri Mkuu Mteule)*

**SPIKA:** Kuna bahasha nyingine tena! *(Kicheko)*

*(Hapa Katibu Alifungua Bahasha ya pili)*

**SPIKA:** Kuna bahasha ya tatu! *(Kicheko)*

*(Hapa Katibu Alifungua Bahasha ya tatu)*

**SPIKA:** Hee! Waheshimiwa Wabunge, hii barua kutoka kwa Mheshimiwa Rais imeandikwa kwa mkono wake yeye mwenyewe, haikuchapishwa. *(Makofi)*

Ameniandikia, Job Ndugai, Mheshimiwa Spika, kwa kifupi kabisa kwamba yeye mwenyewe, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa nafasi yake kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amemteua, amemteua… *(Kicheko/Makofi)*

Amemteua Mbunge wa Ruangwa, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kuwa ndio Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia kwenye utaratibu nilioutoa mwanzoni, naomba nisitishe shughuli za Bunge kwa muda wa dakika 45, halafu turudi hapa ndani tuje tutekeleze wajibu wetu wa Kikatiba.

Wakati huo huo Mheshimiwa Ali Saleh alikuwa ameniambia kwamba kwa dakika hizo chache wale wa Kambi hii nyingine mkutane Msekwa. Nafikiri tumeelewana. Ahsante.

Naomba kusitisha Shughuli za Bunge kwa dakika 45.

*(Saa 3.45 Asubuhi Bunge lilisitishwa kwa muda wa dakika 45)*

*(Saa 4.55 Asubuhi Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU**

**ND. JOHN N. JOEL - NAIBU KATIBU WA BUNGE:** Kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, shughuli inaendelea.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tulipoachia, sasa tunaendelea na zoezi letu la kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu na mtu wa kwanza kumwita ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii kwa mujibu wa kanuni 25(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili niwasilishe hoja ya Serikali kuomba Bunge lako Tukufu limthibitishe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 sura ya pili ya sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatekeleza jukumu hilo la kikatiba, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na karama mbalimbali na hivyo kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ipasavyo kama tunavyomwomba kila siku ya shughuli za Bunge ambapo pamoja na mambo mengine, katika dua yetu tunamwomba Mwenyezi Mungu aibariki nchi yetu idumishe uhuru, umoja, haki na amani, atuongezee hekima na busara sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tufanye maamuzi sahihi yenye manufaa kwa watu wote na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kukupongeza wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kongwa ili uwe Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. *(Makofi)*

Nawapongeza wananchi hao kwa kutuletea Mbunge mwenye uzoefu wa muda mrefu katika utumishi wa umma na Bungeni ambaye hatimaye amechaguliwa na sisi Wabunge wenzake kuwa kiongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) Bunge ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja. Naungana na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wa Tanzania kukutakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu ya kuongoza mhimili huu wa Bunge kwa mafanikio ipasavyo. Unao uzoefu wa kuongoza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, uliingia ndani ya Bunge hili tangu mwaka 2000 chini ya uongozi wa Mheshimiwa Pius Msekwa aliyekuwa Spika na umekuwa ukitekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kuwa Mwenyekiti wa Bunge katika Bunge la Tisa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Samuel Sitta akiwa Spika na Mheshimiwa Anna Makinda akiwa Naibu Spika na kisha kuchaguliwa na Bunge la Kumi kuwa Naibu Spika kazi ambayo uliifanya vizuri chini ya Mheshimiwa Makinda na sasa umepanda cheo na kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nawashauri Wabunge wenzangu tuendelee kukupatia ushirikiano ili uweze kutekeleza majukumu yako ipasavyo kwa mujibu wa katiba, sheria na kanuni za kudumu za Bunge kwa hekima kama ilivyo kawaida yako. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakuwezesha ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika napenda kuchukua fursa hii kwa dhati, kumpongeza Mheshimiwa Anna Makinda, Spika Mstaafu wa Bunge la Kumi, kwa kazi nzuri aliyoifanya kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa mafanikio makubwa. Moja ya mafanikio hayo ni kuanzishwa kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Bajeti ya 2015. Sheria hiyo ya Bajeti pamoja na mambo mengine, inaweka masharti kuhusu kusimamia na kufuatilia mchakato na utekelezaji wa bajeti ya Taifa, kuweka misingi ya sera ya bajeti, mipango na miongozo ya bajeti, mamlaka ya Bunge kuhusiana na bajeti, kuainisha mamlaka na majukumu ya Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Tume ya Mipango na Kamishina wa Bajeti, kuhusiana na uandaaji na upitishwaji wa bajeti ya Taifa, matumizi na utoaji fedha, kuainisha uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Dharura, utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu, usimamizi wa mapato na usimamizi wa Serikali na Taasisi za Umma.

Aidha, sheria hii imeweka masharti unayoitaka Hazina kulipa katika kipindi cha robo mwaka fedha zote zilizotolewa na Bunge kugharamia matumizi ya shughuli za Bunge na Mahakama kwa ajili ya kila robo ya mwaka wa fedha. Sheria hii itawezesha Bunge na Mahakama kuwa na rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na kazi za mihimili hiyo kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Anna Makinda atakumbukwa kwa kutoa mchango wake katika kufanikisha azma hiyo. Namtakia kila la heri katika maisha yake na Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema na maisha ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wote waliokuwa wagombea katika nafasi za Kiti cha Urais, Ubunge na Udiwani. Naomba kuwashauri wote kwa pamoja na bila kujali itikadi za kivyama, kushirikiana kwa dhati kabisa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya manufaa na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa na kukabidhiwa dhamana ya kuongoza nchi yetu akiwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka mitano ijayo. Namtakia kila la heri katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dkt. John Pombe Magufuli anao uwezo wa kumudu majukumu yake ipasavyo, anayo nia na sababu ya dhati ya kuwatumikia Watanzania kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 62(1) ya Katiba, Rais ni sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi Wabunge tunawajibika kikatiba kumpatia ushirikiano stahili ipasavyo, huku tukizingatia kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 33 ya Katiba, Rais ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Kwa majukumu haya ya Rais, sisi Wabunge tunawajibika kikatiba

kumpatia ushirikiano Rais tunapokuwa tunatekeleza majukumu yetu kama Wabunge. Aidha, namshukuru sana kwa kuniamini na kuniteua katika nafasi hii. *(Makofi)*

Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba na kisheria kwa kuzingatia katiba na sheria za nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa viapo vyangu katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa aina zote waliopata nafasi ya kuingia Bungeni. Nawatakieni kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu kwa umma huku mkizingatia na kuheshimu Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge mnapokuwa mnatekeleza majukumu yenu kama Wawakilishi wa wananchi, kwa maslahi ya wananchi wa nchi yetu, kwani katika kiapo chetu, Wabunge wote tunaapa kwamba tutakuwa waaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa mioyo yetu yote na kwamba tutaihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kutoa hoja kwa mujibu wa kanuni ya 25(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013 kuliomba Bunge lako lithibitishe uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani uliofanywa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51, ibara ndogo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina masharti yanayoelekeza kwamba, Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika Jimbo la Uchaguzi anayetokana na Chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au kama hakuna Chama cha Siasa chenye Wabunge wengi zaidi anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba Mbunge atakayeteuliwa kushika wadhifa huo, hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo sasa wote tunafahamu, Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, ni Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la uchaguzi la Ruangwa na anatoka Chama cha Mapinduzi ambacho kwa mujibu wa matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015 na kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndicho Chama chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni. *(Makofi/Vigelele)*

Vilevile kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais amelileta jina hilo la Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa katika Bunge hili Tukufu kwa ajili ya kuthibitishwa.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa dhati kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa ni mtu muadilifu, asiyekuwa na makuu, mwenye hekima na busara nyingi, msikivu wa hali ya juu na mchapakazi hodari atakayemudu majukumu yake ipasavyo katika zama hizi za uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu halali ya kila mwananchi almaarufu, Hapa Kazi Tu! *(Makofi)*

Vilevile kwa taaluma yake ya Ualimu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa ni mtu mwenye uwezo wa kuchambua kwa kina na kupima hoja mbalimbali zinapojitokeza. Aidha, uwezo wake mpana na uelewa wake wa mambo katika kufikia maamuzi, umejidhihirisha katika utumishi wake wa muda mrefu kama Mwalimu wa Shule za Msingi na Sekondari. *(Makofi)*

Mkufuzi wa Vyuo vya Ualimu, Katibu wa Chama cha Walimu Wilaya na Mkoa na hata ngazi ya Taifa alikuwa Mjumbe wa Baraza wa Chama cha Walimu. Ni mwana michezo na mkufunzi wa michezo na hata hapa Bungeni kwa ile *club* ya Bunge *Sports Club* amekuwa mkufunzi wao. *(Makofi)*

Amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya za Rufiji na Urambo, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akishughulikia elimu katika Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa anao uzoefu wa utendaji wa kazi wa kutosha na kwa utumishi wake katika ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha sifa hizi katika Bunge hili Tukufu ili kuonyesha kwamba Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa ana uwezo wa kuyabeba na kuyahimili majukumu yote yanayoendana na wadhifa wa kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama yalivyoainishwa chini ya Ibara ya 52(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za nchi na kanuni za kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa kwa unyenyekevu, heshima na taadhima kubwa, naliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Ruangwa, uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ili awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupitisha Azimio la Bunge. Azimio lenyewe ni kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge la kumthibitisha Waziri Mkuu chini ya Ibara 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 25(2) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUWA, Ibara ya 51(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili ya Sheria za Tanzania, inaelekeza kwamba, kutakuwa na Waziri wa Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atakayeteuliwa na Rais na kwa kufuata masharti ya ibara hii ambaye kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Rais;

NA KWA KUWA, Rais kwa mujibu wa Ibara ya 51(2) amemteua Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano;

NA KWA KUWA, Ibara ya 51(2) inaelekeza kwamba Waziri Mkuu aliyeteuliwa hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio lililoungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano linaazimia kama ifuatavyo:-

Kwamba Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Ruangwa na ambaye ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa Waziri wa Mkuu wa Jamhuri ya Muungano amethibitishwa na Bunge na kwa mujibu wa kanuni ya 25(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2013.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana, tunakushukuru kwa maelezo mazuri sana. *(Makofi)*

Nakushukuru sana kwa maelezo mazuri ya utangulizi ambayo umeyatoa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa ni wakati wa mjadala kuhusiana na hiyo hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nilikuona Mheshimiwa Lukuvi, utafuatiwa na Mheshimiwa Chenge, dakika tatu, tatu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nachukua nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa kwa kuchaguliwa na Wabunge wote kwa kura nyingi kuongoza Bunge hili. Nakupongeza sana na namshukuru sana Mwenyezi Mungu angalau kwa kutuletea Spika kama wewe mwenye uzoefu na uwezo wa kuongoza Bunge letu. Hongera sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Pili, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kumpa maono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kumtuma achukue fomu ya kugombea Urais na kumsimamia mpaka ameshinda kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kitendo hicho ambacho Watanzania wote wamefurahi na kweli Dkt. John Pombe Magufuli ni chaguo la Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia tena Mwenyezi Mungu amempenda tena Dkt. John Pombe Magufuli, amempa maono ya kumteua ndugu yetu, Mbunge wa Ruangwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa awe ndiye Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa hili nalo tunamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kumpa maono hayo Rais wetu kwa kumpendekeza mtu mwenye sifa na kazi hiyo ambayo tunatarajia kumthibitisha hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo za Mheshimiwa Rais, napenda niseme kwamba uteuzi wa leo uliofanywa ni uteuzi makini na sahihi. Mheshimiwa Kassim Majaliwa kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, tunaomfahamu sisi tuliofanya naye kazi; mimi nimefanya naye kazi nikiwa katika mwamvuli wa Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wengi wa zamani tumefanya naye kazi, tunamjua, hata mmoja hawezi kusema amegombana na Mheshimiwa Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Watanzania kwa nafasi mbalimbali ya kusikiliza mijadala na hoja mbalimbali zilizokuwa zinajibiwa au kuwasilishwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa hapa Bungeni au waliopata fursa ya kumwona akitembelea kusimamia shughuli zake huko Mikoani, wanamjua Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwamba, kwanza ni mtu muadilifu sana, lakini pili, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, amejaliwa kuwa na sikio, yaani ni msikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kassim Majaliwa ni mchapakazi. Tumeshuhudia hapa akidhihirisha uwezo wake wa kuyasema na kusimamia maneno yake na kuyatekeleza kwa kufuatilia kwa vitendo katika eneo lake la elimu alilokabidhiwa akiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI anayeshughulikia Elimu.

Kwa hiyo, nataka niwathibitishie hata Watanzania wanaosikia kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa anao uwezo wa kufanya kazi hiyo, nasi tunamwombea Mwenyezi Mungu amsaidie sana Mheshimiwa Rais ili atimize lengo lile kubwa ambalo limekabidhiwa na Taifa baada ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono uteuzi huu kwa kuthibitisha kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa ni mtu anayefaa kwa kazi hii. Nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wote tumpe kura za ndiyo bila kujali itikadi zetu. *(Makofi)*

Huyu ndiye atakuwa kiongozi wa shughuli za Serikali humu ndani ya Bunge, lakini atasimamia shughuli zote za Serikali ambazo sisi Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na ahadi zetu zote tulizoahidi bila kutegemea chama, ndiye atakayezisimamia. Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge wote, tumpe kura za ndiyo ili awe kiongozi wetu, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lukuvi, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Jenister Mhagama nilikuona!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuliweka Taifa letu katika hali hii, kwanza ya amani na utulivu mpaka tunapofika siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefika siku ya leo tukishuhudia matukio makubwa ya Kitaifa katika nchi yetu ikiwemo Uchaguzi Mkuu ambao umemweka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli.

Vile vile tulipoanza Bunge hili, Mkutano wa Kwanza wa Bunge hili la Kumi na Moja tumefanikiwa kumaliza hatua ya awali ya kumweka Spika atakayeendesha Bunge hili la Kumi na Moja. Naungana na Mheshimiwa Lukuvi kukupongeza sana wewe na Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili la leo ni la kikatiba, lakini vile vile ni jambo la kikanuni. Kwa dhati kabisa, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kumsaidia Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kuweza kufanikisha kazi hii ya kikatiba kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ametuletea jina la uteuzi wake wa Waziri Mkuu, ndugu yetu Mheshimiwa Majaliwa. Kwa dhati kabisa, kama wote ni Watanzania, tukifuatilia historia ya utendaji kazi wa Mheshimiwa Kassim

Majaliwa, hakuna atakayesimama hapa na kusema Mheshimiwa Kassim Majaliwa sio muadilifu na ana kashfa katika nchi yetu ya Tanzania. Amejiwekea rekodi nzuri sana ya uaminifu na utendaji kazi uliotukuka ndani ya Serikali yetu, lakini huku akiwawakilisha wananchi wake katika Jimbo lake. Amekuwa mchapa kazi kama ilivyosemwa na Mheshimiwa *AG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamkumbuka Mheshimiwa Majaliwa kwa jinsi alivyokuwa akitimiza maagizo mbalimbali ya Serikali kwa usikivu mkubwa. Mheshimiwa Majaliwa ni kijana na Serikali yetu kwa kasi ya Mheshimiwa Rais, inahitaji Waziri Mkuu wa umri huo wa ujana kukimbizana na shughuli mbalimbali ili kumsaidia Rais kufikia pale tunapofikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inahitaji watu waadilifu kama nilivyosema mwanzo, waweze kusimamia maendeleo yetu na kufanya mabadiliko ya kiutendaji kazi katika Serikali yetu kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. Sina shaka na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote, chaguo hili la Rais ni sahihi. Tuunge mkono hoja hii.

Nina hakika matunda ya kumpata Mheshimiwa Kassim Majaliwa yatajidhihirisha wazi na haraka sana kwa sababu ya sifa alizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, naomba kwa heshima kubwa ya Bunge lako Tukufu, niunge mkono hoja hii na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, tushirikiane kwa pamoja kuunga mkono na kumpitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa ili awe Waziri Mkuu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano na tufanye naye kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia amani na utulivu kwenye nchi yetu, lakini namshukuru zaidi kwa kutupa Rais mchapakazi, muadilifu, Dkt. John Pombe Magufuli na namshukuru zaidi Mwenyezi Mungu kwa kutupa Spika mchapaka kazi, makini, mwenye busara na ambaye anaakisi utendaji kazi unaotoa haki kwa kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru zaidi Mwenyezi Mungu leo hii kwa kutuamsha salama na kumwezesha Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kutupatia jina la mteule wa nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninayo furaha kubwa zaidi kama Mwenyekiti wa muda wa Bunge *Sports Club* na mchezaji wa timu ya Bunge *Sports* kwa miaka mitano iliyopita

ambapo Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim amekuwa Mwalimu kwa kipindi chote hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nina masikitiko makubwa kwa sababu sina uhakika kama Mwalimu wetu, Kocha Majaliwa Kassim Majaliwa ataendelea kujidamka asubuhi kwa nidhamu ile ile aliyokuwa nayo kwa kipindi chote ambacho tumecheza naye na kuja kushiriki nasi mazoezi kwenye timu yetu ya Bunge *Sports Club*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nina furaha kubwa zaidi kwamba Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa amekuwa Naibu Waziri kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ambapo mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Wizara hiyo. Nimefanya naye kazi kwa ukaribu na sikuona kingine zaidi ya uadilifu, umakini, utayari wa kufanya kazi, usikivu, hekima na busara ya hali ya juu kwa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, japokuwa mimi ni mdogo wake, lakini siku zote nikiwa Mwenyekiti amekuwa akiniheshimu na akisikiliza maelekezo yangu na Kamati yangu kwa uaminifu na upendo wa hali ya juu kana kwamba yeye ni mdogo na mimi ni mkubwa. Ni mtu mnyenyekevu na naamini kwa Serikali inayoingia madarakani sasa ya Dkt. John Pombe Magufuli, huyu ni mtu sahihi kabisa kwa nafasi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka na uadilifu wake, sina shaka na uwezo wake wa kuchambua mambo, nina hakika hata yale majibu aliyotupa pale Kampala Mheshimiwa Nassari na wengine wanayakumbuka sana; baada ya siku moja tukio moja lilipotokea, alitoa maelezo ya hekima kubwa sana, mwisho wa siku wote tulicheka kwenye kikao kile. Ni mtu mwenye hekima ya hali ya juu, anayejua kuchagua maneno yake. Nina uhakika Wabunge wa kambi zote tutampa ushirikiano wa kutosha kwa sababu yeye ni msikivu, ni mtu mwenye hekima na busara ya hali ya juu; na ana uwezo wa kunyenyekea kila mtu wa juu yake na wa chini yake.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ninayo heshima kubwa sana kuomba Bunge lako Tukufu kwa sauti moja tuazimie kuunga mkono azimio lililoletwa mbele yetu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuweze kumthibitisha Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa aende kuwa Waziri Mkuu wetu kwenye Serikali inayoingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, nakushuru. Sasa wa mwisho awe Mheshimiwa Andrew Chenge. Mheshimiwa uliyesimama, nimekuona.

**MBUNGE FULANI:** Hakusimama huyo! *(Kelele)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola! *(Kelele)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni miongoni mwa Watanzania zaidi ya milioni 45 ambao siku ya leo tunayo furaha. Tunayo furaha kwa sababu kilio cha Watanzania juu ya maisha yetu, juu ya maendeleo yetu, tulifika mahali tukigeuka kulia, kushoto, mbele nyuma tukawa kama tuko jangwani. Lakini mwaka huu umekuwa ni mwaka wa neema kwa sababu Mungu amesikia na amejibu kilio cha Watanzania. Mungu ametuletea tinga tinga Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao pengine mmepoteza kumbukumbu, mchakato wa kumpata Rais ulikuwa ni mchakato wa Kimungu, ndiyo maana John Pombe Magufuli aliweza kuibuliwa miongoni mwa wana-CCM 42 kwa sababu Mungu aliona huyu ndiye atajibu matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia ni mwaka wa neema kwa sababu wewe mwenyewe umekuwa ni Mbunge mwenzetu, umefanya kazi na sisi, umeendesha Bunge hili kwenye kiti ulichokikalia leo kama Spika, ni Mungu pia amejibu kilio cha Wabunge kwamba tulikuwa tunamtafuta Spika ambaye ataendesha Bunge hili kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nataka niwaambie Watanzania wenzangu na Wabunge wenzangu mnaonisikiliza, Mheshimiwa Rais ambaye Mungu alimwona ni mwema, naye leo tumeshuhudia anazaa chema. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa wenzangu ambao ni wasomaji wazuri wa Biblia watakumbuka pale ambapo Mungu alimtuma Nabii Samweli aende nyumbani mwa Yese kwamba ndimo atakapokwenda kumpaka mafuta atakayekuwa Mfalme wa Wayahudi. Alipofika nyumbani mwa Yese, alikuta ana watoto wengi na wengi walikuwa ni wale wenye majina makubwa, lakini kila Yese alipokuwa anasema kwamba wewe njoo hapa, aliwakataa; na baadaye yule ambaye hakutarajiwa kabisa, tena mtoto mdogo alikuwa anachunga ng'ombe, Daudi, ndiye akasema kwamba haka ka-Daudi haka ndiko nimetumwa kuja kukapaka mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Majalilwa Kassim Majaliwa ni miongoni mwa wanadamu ambao hawazaliwi kila wakati, hawazaliwi kila mahali na hawapatikani kila mahali, popote, ni miongoni mwa watu wachache sana.

Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa leo tumeshuhudia pasipo kutarajia, ameweza kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa nchi yetu. Sote tunamfahamu, Mheshimiwa Majaliwa ni mtu makini, ametulia na ndiyo maana mambo mawili ninayomshuhudia, wenzangu tuliokuwa kwenye Kamati ya *LAAC*, ya kusimamia mahesabu ya Serikali za Mitaa, tumepata ushirikiano mzuri sana wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa; na hasa pale tulipokuwa tunasema watumishi wanaovurunda wasihamishwe, washughulikiwe mahali walipo; na ndiyo Kauli ya Mheshimiwa Rais, kwamba atakayevuruga mahali alipo naye hapo hapo ni kwa heri. Kwa hiyo, Majaliwa atakuwa ni miongoni mwa wanaotekeleza "Hapa Kazi Tu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Majaliwa katika ufuatiliaji ni nambari moja. Nilipokuwa na tatizo la Walimu wa Shule ya Msingi Nambaza, shule ambayo iko pembezoni kabisa kule Mwibara, Walimu wale walipofanyiwa mambo ya ushirikina, ni Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa aliyenipigia simu usiku wa manane akifuatilia matatizo ya Walimu hawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nani kama Kassim Majaliwa?

**WABUNGE:** Hakuna!! *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Nani kama Kassim Majaliwa?

**WABUNGE:** Hakuna!! *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, wakati nakwenda kukaa, nawaomba Wabunge wenzangu, kama kuna mtu ambaye sasa tutakwenda aleselema alija, mchaka mchaka kuikimbiza nchi yetu wananchi wapate neema, wapate maendeleo, kuanzia kesho baada ya kuapishwa, ni jembe la pili baada ya Magufuli, ni Majaliwa Kassim Majaliwa. Tumpe kura zote kabisa za ndiyo! *(Makofi/Vigelegele)*

Ndiyo maana nimekuona wewe Mheshimiwa Saed Kubenea, nimekuona Mheshimiwa Mbatia; wakati wanatamka jina la Majaliwa Kassim Majaliwa, niliwaona nyote mnafurahi na kupiga makofi kwamba tumepata jembe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, Wabunge tumpitishe kwa kura zote za ndiyo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Mheshimiwa, nilitaka nikupe nafasi uchangie kabisa, au unataka taarifa kwanza?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Taarifa!

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Mwibara aliyemaliza kuongea muda huu, ametumia jina langu vibaya. Sikupiga makofi, sikushangilia na ninazo hisia zangu. Naomba afute hiyo kauli yake kwa kutumia jina langu vibaya katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Naomba tusiendeleze malumbano hayo, tuanze kwa *spirit* ile ambayo tumeisema. Ulisimama, nilitaka nikupe dakika za kuchangia au! Wakati ule mliposema kwamba kwenye kambi hii Mheshimiwa Kubenea naye angependa kuchangia, nilitaka nimpe nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ni Mheshimiwa Msigwa!

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Msigwa, sio Mheshimiwa Kubenea?

Mheshimiwa Kubenea naomba haya mambo ya Mheshimiwa Lugola tuyaache tu, ni utani tu wa humu ndani.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru, lakini naomba kabla sijachangia, ni lazima Mheshimiwa Mbunge afute kauli yake…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu huo ndiyo utaratibu wa kibunge na ndiyo msingi wa majadiliano Bungeni, kwamba Mbunge asitumie jina la mtu mwingine bila ridhaa yake na Mheshimiwa Mbunge ametumia jina langu vibaya.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, nakupa dakika tatu kama nilivyowapa wengine. Katika dakika tatu hizo, sahihisha hayo yaliyosemwa na Mbunge mwenzako kama siyo sawa sawa. Naomba uzitumie, kama huzitumii niwape

watu wengine; kwa sababu nakupa fursa sasa usahihishe uweke jina lako vizuri linavyopaswa kuwa. Mheshimiwa Kubenea!

*(Hapa Mheshimiwa Saed A. Kubenea Alikaa Kimya)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chenge! Tunaendelea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, sasa si alisimama mtu!

**SPIKA:** Mheshimiwa Chenge, endelea kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nami niongeze jina langu katika orodha ya Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuongea katika kuunga mkono hoja iliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ya kuthibitisha uteuzi wa Mteule wa Mheshimiwa Rais kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Nasema naunga mkono hoja hiyo mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kukupongeza wewe kwa imani ambayo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili wameonesha kwako kupitia kura zao. Hongera sana na tunaamini uzoefu na uwezo ulionao kwa nafasi hiyo, kweli tumepata Spika ambaye ataendeleza mazuri ya kuboresha na kuimarisha Bunge letu. Hongera sana. *(Makofi)*

Tatu, nami niungane na Watanzania wenye mapenzi mema na nchi yetu kwa uamuzi wao kupitia kura zao za kumchagua Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na mwenza wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunawapongeza kwa sababu imani hiyo ni kwa Tanzania, ni kwa CCM na sera zake za kuendelea kuwapatia matumaini Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo, katika hoja iliyo mbele yetu, napenda nai nithibitishe katika kuunga mkono jina lililoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Rais la Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Nimemfahamu huyu kijana tangu alipoteuliwa kuwa *DC,* nakumbuka ilikuwa mwaka 2006. Nimekutana naye Mikoani na niliona dalili nzuri kwake. Ni kijana msikivu sana, mnyenyekevu, mpole, hana makuu na tumeona pia alipochaguliwa na wananchi wa Ruangwa kuwa Mbunge wao, amepewa nafasi ya Unaibu Waziri; jinsi anavyojibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge ya msingi na ya nyongeza, unaona ana uelewa, ana umakini na anafahamu sana kufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sishangai kama kweli imempendeza Mheshimiwa Rais kama ilivyompendeza, kuleta jina la Mheshimiwa Majaliwa kuwa Mteule kwa nafasi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuungane bila kujali itikadi ya vyama vyetu, tumpatie kura zetu zote za ndiyo katika kumthibitisha ndugu yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa James Mbatia nakuona umeshika Kanuni.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutumia Kanuni ya 68(7) ya mwongozo wako; na ili kuokoa muda wa Bunge, naomba nisiisome.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge Kangi Lugola alivyokuwa anachangia, ametaja jina langu na kuweka kwenye *Hansard*, kitendo ambacho mimi sijakifanya na kuwaaminisha Watanzania nimefanya kitendo hicho. Ningeomba afute kauli yake ili kuleta hali ya amani na utulivu Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola jambo hili ni jepesi sana, hatuna sababu ya kuliendeleza. Ulisema kwamba uliona wakicheka na kupiga makofi, basi inaelekea labda giza giza hili kidogo na nini; weka sawa tu hilo jambo ili tuweze kuendelea. *(Kicheko)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, makofi waliyokuwa wanapiga pengine hawakuwa pamoja na sisi, walikuwa wanashangilia kitu kingine… *(Kicheko/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Ondoa!

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba niyaondoe hayo maneno. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru sana. Baada ya kufikia hatua hiyo, sasa namwomba Katibu atupe maneno kidogo hapa ya kuhusu utaratibu. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya mjadala huu, hoja hii kwa kawaida inaamuliwa kwa kura ya siri. Kwa hiyo, utaratibu wetu wa kura ya siri ni kwamba kila Mbunge atapewa karatasi yenye jina la Waziri Mkuu Mteule, utaweka alama ya vema na baada ya hapo

karatasi hizo zitakusanywa. Watapatikana Mawakala kutoka miongoni mwa Wabunge ambao Spika atakuwa ameamua, kura zitahesabiwa, zitarejeshwa hapa, tutasoma matokeo. Kura nyingi zitakazopatikana ndizo zitakazokuwa zimemthibitisha Waziri Mkuu Mteule.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako tunaomba tufanye zoezi la kupiga kura.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaingia katika zoezi la kupiga kura. Kwa hiyo, Katibu, naomba sasa tuendelee na utaratibu kadri ulivyopangwa. Wale watu walioandaliwa muanze kusogea, Maofisa mwingie hapa pamoja na vifaa vyenu. *Sergeant-At-Arms,* naomba utupigie kengele huko ili Waheshimiwa Wabunge ambao wako nje waweze kurudi ndani na pia impatie nafasi Katibu kuweza kujua akidi yetu na idadi ya watu waliopo humu ndani.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu!

**MBUNGE FULANI:** Wakati Mheshimiwa Katibu anaeleza hapa, alieleza kwamba karatasi zitakazokuja zitakuwa na sehemu ya kuweka alama ya vema tu kwa *assumption* kwamba hapatakuwa na watu ambao wanataka kufanya vinginevyo. Sasa wale ambao wanataka kufanya vinginevyo, iko namna gani kwenye karatasi? Tutafanya hivyo au ni ile alama ya vema tu moja kwa moja? Kwa sababu nilifikiri labda kuna viboksi. Viboksi viwili viwepo! Aunaomba ufafanuzi.

**SPIKA:** Kwani Mheshimiwa kuna anayetaka kufanya vinginevyo tena! Si tumeelewana hapa ndani!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, tupo kila mtu na…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nimekuelewa! Katibu fafanua! *(Kicheko)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli. Kutakuwa kuna aina mbili. Unaweza ukaweka alama ya ndiyo au hapana. Mbele ya maneno hayo unaweza ukaweka chaguo lako, kwa sababu huo ndiyo utaratibu wa kidemokrasia.

**SPIKA:** Kama alivyoeleza Katibu karatasi utaipata, iko tu vizuri ina jina la anayependekezwa na kuna viboksi viwili; cha kwanza kinasema "ndiyo" na cha pili kinasema "hapana." Wewe utaweka tiki mbele ya kimojawapo katika hivyo viwili. Nadhani imekaa vizuri jamani, au siyo! Ahsante.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu! Tuwe tunataja na majina yetu; bado tupo wageni tulio wengi!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naitwa Lusinde, Mbunge wa Mtera.

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika kuhusu utaratibu! kwa kuwa tunajua sasa kuna viboksi viwili cha hapana na cha ndiyo, tafsiri yake kwa nini isiwe hata atakayesema hapana, hakuna mwingine isipokuwa Majaliwa Kassim Majaliwa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Ahsante. Nawe jitambulishe pia!

**MHE. WILFRED M. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naitwa Wilfred Rwakatare kutoka Bukoba *Town*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu ambao umetolewa hivi sasa, na kutokana na mwenendo ambao unaendelea hivi sasa kwa taswira yake, tunaomba kujua utaratibu utakaotumika wakati wa kuhesabu kura kuhusiana na uwakala. Kwa sababu tumeshaona taswira zitakuwa mbili, kuna wenye utashi wa "hapana," kuna wenye utashi wa "ndiyo" na hasa tukizingatia hata tabia iliyoonekana kwenye Uchaguzi Mkuu. Ahsante *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa utaratibu uliopo, Mawakala watateuliwa na Spika. Katibu, tafadhali sasa tuendelee.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu. Idadi ya Wabunge Kikatiba ni 394, idadi ya Wabunge waliosajiliwa ni 369 ambao ndio wapo kwa sasa. Akidi kwa mujibu wa Kanuni ya 77 ni Wajumbe 184. Wabunge mliopo sasa ndani ya ukumbi huu ni 351. Kuna uhalali wa kufanya zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa ridhaa yako, tuendelee na zoezi la kupiga kura. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu, tulichelewa kidogo kwa ajili ya kupata idadi ya Wabunge maana yake wengine wanahamahama na nini, ikawa inaleta taabu kidogo. Sasa tugawe karatasi za kura. Hili ni zoezi la haraka tu mara moja. Masanduku ndiyo hayo yapo tupu! Naomba tufanye zoezi hilo *chap chap!* Kila mmoja wetu apate karatasi moja, ukishapiga kura, ikunje vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mkishapiga kura naomba msitoke nje ili tuendelee na zoezi la uchaguzi wa Naibu Spika moja kwa moja ili tuweze kuokoa muda. Wakati kura hizi zikienda kuhesabiwa, sisi tuendelee na kuwasikiliza Wagombea wa Unaibu Spika.

Waheshimiwa Wabunge, ukishapata karatasi yako upige kura. Pawe na umakini katika ugawaji wa karatasi zisije zikagawanywa zaidi ya mmoja kwa kila Mbunge. Naomba Maofisa wangu tujipange kukusanya hizo kura *chap chap!* Kama kuna Mheshimiwa yeyote ambaye hajapata karatasi ya kura, ungeweza kusimama hapo ulipo ili ufikishiwe karatasi kwa haraka. Naomba Maofisa wangu mharakishe karatasi maeneo hayo ambayo Waheshimiwa Wamesimama. Wahini katika maeneo hayo tuokoe muda. Kila anayepata karatasi akae, kama hujapata, simama.

Ahsante. Naona wote sasa tumepata karatasi za kura, ni zoezi fupi tu la haraka haraka, naomba tupige kura na zianze kukusanywa moja kwa moja.

Waheshimiwa Wabunge, tuwape vijana wetu hizo karatasi za kura. Naomba kura zikusanywe. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye hajatumbukiza kura yake kwenye *box*, tunaomba afanye hivo. Kuna moja iko huku! Nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote tayari mmeshamaliza. Naomba ifuatwe hiyo kura halafu mje msimame hapa.

Sasa tunaelekea kwenye kwenda kuhesabu na kwa hiyo, nawaomba Kambi Kuu mbili katika kuwashirikisheni, kila upande utoe Wabunge wawili wawili. Mheshimiwa Mbatia, Wabunge wawili; mmoja mwanaume, mmoja mwanamke.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, tunaomba kumteua Mheshimiwa John Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini, pamoja na Bi Riziki kutoka Viti Maalum *CUF*.

**SPIKA:** Ahsante. Wabunge waliotajwa naomba waje mbele.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Wabunge wawili; mmoja mwanaume mmoja mwanamke!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa upande wa Chama Tawala, Mheshimiwa Amina Makilagi atawakilisha Wabunge wanawake na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni atawakilisha Wabunge wanaume. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Naomba Mheshimiwa Chegeni na Mheshimiwa Makilagi msonge hapa mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa kwa ruhusa yenu, hii timu iweze kwenda mahali palipoandaliwa na Katibu kwa ajili ya kuendelea na zoezi la kuhesabu kura; naomba muanze kuelekea kwenye eneo husika. *(Makofi)*

*(Hapa zoezi la kuhesabu kura lilianza katika eneo husika)*

**SPIKA:** Sasa Katibu tuendelee na Ajenda inayofuata.

**UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natumaini tuko pamoja. Sasa tunaingia katika zoezi la Uchaguzi wa Naibu Spika. Namkaribisha Katibu wa Bunge sasa atueleze kuhusu yatokanayo na zoezi hilo.

Katibu, tuendelee!

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa Kanuni, Kiti cha Naibu Spika kilikuwa wazi siku Bunge lilipoitishwa. Kwa sababu hizo hizo, nilitoa taarifa kwenye Gazeti la Serikali na kuchapishwa tarehe 6 Novemba kwenye Tangazo Namba 515 nikiainisha kwamba nafasi hiyo itakuwa wazi na kwamba, wenye nia ya kugombea nafasi hiyo wawasilishe majina ifikapo tarehe 18 Novemba, saa 10.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, hadi saa 10.00 jioni siku hiyo ya tarehe 18, nilipokea majina mawili ya Wagombea wakiwa wamependekezwa na vyama vyao, ambayo naomba niyasome.

Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya amependekezwa na Chama cha Wananchi *CUF* na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu amependekezwa na Chama cha Mapinduzi, yaani *CCM. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wagombea wote wamekidhi vigezo na tunawaleta mbele yenu ili mweze kuamua nani anafaa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika Taratibu za Uchaguzi. Kila Mgombea atatakiwa kufika mbele yenu, yaani ninyi Waheshimiwa Wabunge, kujieleza kwa dakika tatu, kuulizwa maswali kama yapo na kuyajibu na baadaye kuomba kura.

Zoezi hilo likikamilika, kila mpiga kura, kwa maana ya ninyi Wabunge, mtapewa karatasi ya kura yenye majina mawili na mtapaswa kumpigia kura Mgombea mmoja tu kati ya hao wawili, kwa kuweka alama ya vema katika kisanduku mbele ya jina la Mgombea unayempenda.

Wabunge wenye mahitaji maalum watapata msaada wa kuweza kupiga kura katika mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, kila Mgombea atakuwa na haki ya kuteua Mbunge atakayemwakilisha katika zoezi la kuhesabu na kusimamia kura. Zoezi la kuhesabu kura litafanywa na Watendaji wa Sekretarieti walioandaliwa kwa ajili hiyo na kusimamiwa na Wabunge, yaani Mawakala.

Mheshimiwa Spika, baada ya kura kuhesabiwa, Msimamizi wa Uchaguzi atatoa taarifa kuhusu matokeo ya kura hizo. Mgombea atakayekuwa amepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa mshindi wa Kiti cha Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, narejesha kwako ili sasa Wagombea kwanza watoke nje; anaingia mmoja na atajieleza mbele yenu, ataomba kura na atulizwa maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kurejesha.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu kwa maelezo. Mpaka hapo Waheshimiwa Wabunge kuna neno lolote? Nadhani tumeelewana eeh? Ahsante!

Basi namwomba Mheshimiwa Tulia Ackson atoke nje. Mheshimiwa Tulia atoke nje! *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Dkt. Tulia A. Mwansasu aliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Namwomba Mheshimiwa Magdalena Sakaya moja kwa moja achukue *stage* na kuomba kura. Hapa mbele! *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu siku ya leo kwa ajili ya shughuli muhimu ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, jina langu naitwa Magdalena Sakaya, ni Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jimbo la Kaliuwa, Chama Cha Wananchi – *CUF,* Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nipo mbele yenu asubuhi ya leo kuweza kuomba ridhaa yenu, kuomba imani yenu, mnichague kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungani wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu yangu ni ya Chuo Kikuu, ninao uzoefu wa kutosha. Nina uzoefu wa kutosha ndani ya Bunge hili kwa miaka 10, nina uzoefu wa kutosha katika kuongoza sekta nyingine kwa miaka 10. Kwa hiyo, nina uzoefu wa uongozi wa miaka 20 ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeomba nafasi hii ya Naibu Spika kwa kuwa najua kwamba ninao uwezo, ni kiongozi ambaye najiamini; ni kiongozi ambaye najitambua; ni kiongozi ambaye ninathubutu mara zote katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi yetu yanasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Bunge letu linahitaji viongozi makini na ninakupongeza sana kwamba tunaye tayari Mheshimiwa Spika ambaye ni Jemedari, ataenda kuifanya kazi yetu vizuri. Kwa hiyo, unahitaji pia kuwa na Naibu Spika msaidizi wako mwenye uwezo mzuri, anayejua shida za Watanzania, aliyejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunaweza kulisaidia Taifa letu liweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa pamoja bila kujali chama, itikadi, jinsia, wote mnipe kura zenu za "Ndiyo" niweze kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. Ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mgombea! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa ni wakati wa maswali mafupi endapo yapo. Mheshimiwa anayetaka kuuliza swali atasimama pale alipo. Kama hakuna maswali, haya!

**MBUNGE FULANI:** Maswali yapo.

**SPIKA:** Maswali yapo eeh!

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**SPIKA:** Haya, tuanze na dada pale, halafu kaka. Upande huu hakuna swali, eeh?

**WABUNGE FULANI:** Yapo!

**SPIKA:** Atamalizia dada pale! Haya!

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, kwa jina naitwa Angela Jasmine Kairuki. Napenda nimwulize Mgombea; Mheshimiwa Spika anatokana na Chama cha Mapinduzi, yeye ni Mgombea wa Chama cha *CUF;* atueleze atakapochaguliwa atawezaje kufanya kazi na Spika ambaye sio wa Chama chake?

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! *(Kelele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na uvumilivu, tumpe nafasi Mgombea aweze kujibu swali. Mheshimiwa Sakaya, jibu swali! *(Kelele)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, unaniruhusu nijibu?

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru dada yangu Kairuki kwa swali ambalo ni zuri sana. Nchi yetu ina mfumo wa vyama vingi, Bunge letu ni Bunge la vyama vingi. Ndani ya Bunge letu, vyama tumetumia kama njia za kuingilia kwenye Bunge hili, lakini tunafanya kazi kama *team. (Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu na matumaini yangu kwamba kila Mbunge aliyepo hapa Bungeni anafanya kazi kwa ajili ya Watanzania ambao ndio tegemeo letu. Kwa hiyo, nitafanya kazi na Mheshimiwa Spika aliyechaguliwa kama Naibu Spika, kuhakikisha matarajio na malengo ya Watanzania yanatimia bila kuangalia Chama. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa hapo, la kwako litakuwa la tatu. Swali la pili kule kwa Mheshimiwa Gekul! Jitambulishe kwanza!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali. Naitwa Gekul Pauline ni Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgombea umetuambia una uzoefu na umekuwa Mbunge kwa awamu tatu sasa. Unafahamu kwamba, Taasisi ya

Bunge ni Taasisi kubwa ambayo inawakilisha maoni ya wananchi wengi, lakini kwa muda mrefu mawazo katika Bunge hili yamekuwa hayatekelezwi vizuri na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali; utatumiaje uzoefu wako huo mzuri kuunganisha Bunge na Serikali ili waweze kutimiza yale ya wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Mgombea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Gekul.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba sasa hivi tunayo Serikali mpya ya Awamu ya Tano na pia tunalo Bunge jipya ambalo ni Bunge la Kumi na Moja. Katika miaka 10 ambayo nimekaa ndani ya Bunge, yako mambo ambayo tulikuwa tunajua kabisa kama ndani ya Bunge hayakutakiwa kuwepo, lakini yalikuwepo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nadhani tuna sura mpya za Wabunge wengi, tuna sura mpya ya Mheshimiwa Spika, tutakuwa na sura mpya ya Naibu Spika. Ni matarajio yangu na ni imani yangu kwamba yale yote ambayo yanatarajiwa ndani ya Bunge, kama Mheshimiwa Spika akisimama imara na Naibu Spika akisimama imara, Bunge likawa imara, Serikali ikawa imara, tunakwenda kutoa matarajio makubwa na matumaini kwa Watanzania ambao wanatutegemea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho! Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa pale!

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami ningependa kumwuliza Mgombea swali moja.

**SPIKA:** Taja jina.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini. Ndiyo mara yangu ya kwanza kuingia humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa huko nje kabla ya kuingia humu ndani nimeshuhudia mara kadhaa baadhi ya Wabunge wakisusa na kutoka nje. Sasa naomba kumuuliza Mgombea, utatumia hekima gani za kiuongozi kuhakikisha kwamba, hata kama kuna Wabunge hawaridhishwi na mwenendo wa humu ndani, unawashawishi kubaki ili waendelee na mijadala? Kwa sababu kwa kubaki ndani ndiyo tunawatendea haki wananchi na kwa kutoka nje hatuwatendei haki wananchi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mgombea!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru pia kwa swali zuri.

Mheshimiwa Spika, humu ndani tunaongoza Wabunge. Wabunge ni watu wenye uelewa wa kutosha, ni watu waliokuja hapa kwa matarajio na malengo, ni watu ambao hawatakiwi kuburuzwa, ni watu ambao wanatakiwa kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona Wabunge wanatoka nje, ina maana kuna vitu ambavyo hawakufurahishwa navyo. Nchi yetu inaongozwa na Katiba. Katiba inatoa namna mbalimbali ya watu ku-*express feelings* zao pale wanapoona hawakutendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nategemea Bunge hili litakuwa na ushirikiano wa hali ya juu, umoja wa hali ya juu, mshikamano wa hali ya juu, tuone kwamba sasa tunaenda kuwa wamoja na kwa nia moja kwa pamoja tukasimame kwa maslahi ya Watanzania tuache Vyama pembeni.

Mheshimiwa Spika, pia viongozi wa Bunge wakiwa imara, nina imani kabisa Wabunge wetu watakwenda kuwa na umoja. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mgombea. Maswali matatu yamekamilika. Sasa nakuruhusu utoke nje ili tuweze kumruhusu mwenzako naye aingie. Unatakiwa utoke nje sasa. *(Makofi/Vigelele)*

*(Hapa Mhe. Magdalena H. Sakaya aliondoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Namwomba Mheshimiwa Tulia Ackson aingie ndani. Mheshimiwa Tulia Ackson aingie ndani!

*(Hapa Mheshimiwa Tulia Ackson aliingia ndani ya Ukumbi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tulia Ackson mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge ambao ni wapiga kura kwa nafasi ya Naibu Spika na wewe ni Mgombea. Nakupa dakika tatu ujieleze uweze kuomba kura na kama kuna maswali matatu ya kuuliza, utayajibu. Karibu sana ujieleze.

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Niliyesimama mbele yenu, naitwa Tulia Ackson. Nakupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo ambazo zimeashiria ujuzi, weledi na uzoefu wako katika kazi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika kwa taaluma mimi ni Mwanasheria, nimefanya hiyo kazi kwa muda wa miaka 14; na pia kwa wale Wabunge ambao walikuwepo kwenye Bunge la Katiba, nilikuwa Mjumbe. Kwa hiyo, nilishiriki katika kutengeneza kanuni ambazo ziliendesha Bunge la Katiba vizuri… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hata elimu, unasoma!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, nimesimama…

**SPIKA:** Naomba nimlinde Mgombea. Endelea kujieleza Mgombea!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Waheshimiwa nadhani mnipe nafasi ya kuongea. Kusoma ni haki yangu, nami ni Mwanasheria, nasi huwa tunasoma. *(Kelele/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ooooooh! *(Kelele/Makofi)*

**SPIKA:** Usiwafuate wao, endelea kujieleza Mheshimiwa!

**MBUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, nimesimama mbele yako na mbele ya Wabunge ili niweze kugombea nafasi ya Naibu Spika. Nagombea nafasi hii kwa sababu ninajiamini, ninao uwezo na kazi inayoenda kufanyika…*(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Hamna kitu! *(Makofi/Kelele)*

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Kazi ya Naibu Spika pamoja na Spika ni kutafsiri kanuni za Bunge, Sheria za nchi na pia katiba. Nami hayo ndiyo maeneo ambayo nimebobea kikazi. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesimama mbele yako na mbele yenu Wabunge kuomba kura zenu kwa ajili ya hii nafasi ya Naibu Spika. Nami naahidi kwamba nitawatumikia wote bila kujali vyama vyetu, bila kujali taaluma za watu, bila kujali hali ya mtu, mwanamke, mwanaume, Mbunge kijana, Mbunge wa umri wa kati na pia Mbunge mwenye umri mkubwa. Nitakuwa Mtumishi wa Wabunge wote kwa pamoja. *(Makofi/Kelele)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu, mimi nitakuwa mtumishi wenu. *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Umepata! *(Makofi/Kelele)*

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mgombea ameshajieleza. Sasa ni wakati wa maswali kama yapo. Naomba maswali hakuna!

**WABUNGE FULANI:** Yapoooo! *(Makofi/Kelele/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa naona umeniruhusu nisimame…

**SPIKA:** Naona wote mliosimama ni wanaume wote. Dada ni mmoja tu! Nimpe dada pale! Mheshimiwa una nafasi ya kuuliza swali.

**MBUNGE FULANI:** Esther!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nashukuru sana, sana, sana!

**SPIKA:** Jitambulishe!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naitwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Jimbo Tarime Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mgombe wa nafasi ya Unaibu Spika, Ndugu Tulia, tunatambua kwamba alikuwa ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kipindi hicho hakutakiwa awe mwanachama wa Chama cha Mapinduzi au Chama chochote kile. Kulikuwa kuna kesi ya uchaguzi na alihusika na wote mnajua ni maamuzi gani yalitoka. Lakini baadaye… *(Kelele)*

Niache niulize swali. Naadaye… *(Kelele)*

Tulieni, tulieni kidogo! Baadaye aliendelea akatoa yale maamuzi na ikasikika. *(Kelele)*

Msikilizeni, atajibu jamani! *(Kelele)*

Mheshimiwa Spika, swali langu…*(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Jamani namlinda muuliza swali. Nenda kwenye swali moja kwa moja. *(Makofi/Kelele)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Swali langu sasa…*(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Hayo ni majungu, siyo swali! *(Makofi/Kelele)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Leo unaomba nafasi ya Unaibu Spika; iwapo ikiwa mtendaji wa Serikali tena nafasi nyeti sana, lakini tayari ulikuwa unachukua *side* ya CCM wakati unajua kabisa sheria ndiyo inatafsiri mustakabali wa nchi yetu ndiyo inatoa haki. Utatuaminisha vipi sasa tukikupa nafasi ya Unaibu Spika…*(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Majungu Spika! *(Makofi/Kelele)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Utatuaminisha vipi sasa tukikupa nafasi ya Unaibu Spika hauta-*side* na Chama cha Mapinduzi ukaacha kusimamia maslahi ya nchi yetu kuhakikisha kwamba Bunge hili linasimamia Serikali ili kuhakikisha tunatekeleza mustakabali wa nchi yetu? Tutakuamini vipi hautachukua *side* na ikizingatia kwamba umekuja kwa mlango wa nyuma? Ahsante sana. (*Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Majungu siyo mtaji. *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Maneno ya mwisho nayafuta kama Spika. Amekuja kihalali, hakuna cha mlango wa pembeni wala dirisha. Mheshimiwa Tulia, jibu swali hilo.

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Esther Matiko kwamba nilichukua fomu nikiwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nilichukua fomu za kugombea USpika na kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 67 na Ibara ya 72, zikisomwa pamoja, nafasi…*(Makofi/Kelele)*

**WABUNGE FULANI:** Rudiaa! *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Naomba tumsikilize arudie. *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Apelekwe shule huyo! Apelekwe shule! *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Hili Bunge linafanywa sasa hivi kama Bunge la Katiba! *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili tumsikilize vizuri naomba arudie tena kidogo vile vifungu hatukuvisikia vizuri. Mheshimiwa Tulia endelea kujibu. *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Mchukue Esther, umpeleke shule!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Ibara ya 67(2)(g) inanisema mimi kama Afisa Mwandamizi wa Serikali na Ibara hiyo inaongelea sifa za kuwa Mbunge. Wakati nikichukua fomu, Spika anaweza

kuwa Mbunge au mtu mwingine yeyote mwenye sifa za kuwa Mbunge. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 72 inasema hivi, "Afisa Mwandamizi wa Serikali anakoma kuwa kwenye huo uongozi kama akigombea nafasi akiwa *candidate.*" Sasa *candidate* ni mpaka uwe umepita kwenye mchakato. Kwa hiyo,… *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Peleka shule hao!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Kwa hiyo, mimi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuendesha kesi, ndivyo tafsiri ya kifungu hicho cha 104 kwamba kinakataza mikutano. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, swali la pili.

**MBUNGE FULANI:** Siyo swali lililoulizwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saddiq!

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa jina naitwa Suleiman Saddiq, Mbunge wa Mvomero. Naomba kumwuliza swali moja.

Mheshimiwa Mgombea, nimepitia *CV* yako, nimeona umebobea sana kwenye taaluma yako ya sheria. Nimeridhika na hilo na tunahitaji Naibu Spika Mwanasheria, nakupongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Swali langu: Je, utaitumiaje sheria ambayo unayo, taaluma yako na weledi wako kutoa elimu ya ziada kwa wale ambao hawajui lolote ndani ya Bunge hili ili waweze kuelimika kupitia nafasi yako? Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mgombea Tulia Ackson!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali la Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwa nafasi ya Naibu Spika akimsaidia Spika, mojawapo ya kazi za kufanya ni kutafsiri kanuni, Katiba na sheria zilizopo ili kuweza kutenda haki kwa makundi yote yaliyoko humu ndani kwa ajili ya faida ya Taifa hili. Kwa hiyo, nitasaidia Bunge hili na Wabunge wote kwa ajili ya kufanya kazi zile ambazo wametumwa na wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, nilikuona.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Samahani sana Mheshimiwa Spika, bado nilikuwa Bunge la Kumi, samahani sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa mgombea, wewe ni Mwanasheria mbobevu na umepitia fursa nyingi ikiwemo kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa nchi yetu hii. Naamini unafahamu Katiba kama ulivyoeleza pamoja na kanuni zinazoendesha uongozaji wa nchi pamoja na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mgombea wakati unatoa maelezo yako, umesema wazi kabisa kwamba unapogombea nafasi yoyote na tafsiri iliyotoka kwenye ofisi yako na Msajili Mkuu wa Vyama, nafasi ya Uspika watu wanagombea na Msajili Mkuu alipeleka barua kwenye Vyama vya Siasa, wakati huo wewe ukiwa Mwanasheria Mkuu; na Sheria ya Nchi inakata Watendaji wa Serikali kuwa na muhimili wa Chama cha Siasa. *(Makofi)*

Sasa sina nia mbaya na wewe, swali langu ni kwamba, lini ulichukua kadi ya Chama cha Mapinduzi ili ugombee nafasi ya Uspika na baada ya kujiengua, ukapata nafasi ya kuja kugombea nafasi ya Unaibu Spika. *Tell us! (Makofi)*

**SPIKA:** Bado napima hili swali ni swali kweli au? *(Kelele)*

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeeh! Ni swali! *(Kelele/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tulia, maelezo!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge kama ulivyosema kwamba mimi ni Mwanasheria, Katiba nimeisoma; Sheria zinazohusu Utumishi wa Umma nimezisoma; Kanuni zake pia nimezisoma. *(Makofi/Kelele)*

Nasema hivi, kanuni nimezisoma, Katiba nimeisoma, na sheria nimezisoma… *(Kelele)*

**WABUNGE:** Jibu swali! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Lini umechukua kadi? Jibu swali! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Jibu swali, jibu swali!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunamzonga Mgombea! Ni vizuri tukamsikiliza maelezo yake. Mbona ninyi mnapouliza maswali mnasikilizwa? Mnapotakiwa kupata majibu mnakuwa hamna subira? Kwa hiyo, naomba utilivu tumsikilize Mgombea afafanue, atoe majibu kwa swali alilopewa. Nadhani tunaelewa katika hilo jamani eh!

**MBUNGE FULANI:** Tunaelewana!

**MBUNGE FULANI:** Ameingia CCM lini?

**SPIKA:** Malizia majibu!

**MHE. DKT. TULIA ACKSON:** Mheshimiwa Spika, yako makundi matatu kwenye Katiba ambayo yanakatazwa kuwa wanachama wa vyama vya siasa; na hayo makundi yametajwa kwa uwazi kabisa. Kundi la kwanza ni watu wa majeshi. Katiba inasema Wanajeshi ni akina nani? Ni Polisi, wanaofanya kazi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi na…*(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Jamani sikilizeni! *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Umeingia CCM lini? Jibu swali! *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Wape shule. *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Kwa kuwa tayari maswali yote matatu yameshaulizwa na Mheshimiwa Mgombea ameshajibu kwa ufasaha…*(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Wape shule hao! *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Sasa namruhusu Mheshimiwa Tulia kurudi katika Kiti chako. *(Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli wewe Spika! *(Makofi/Kelele)*

**SPIKA:** Namruhusu Mheshimiwa Magdalena Sakaya, naye arudi. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Unabebwaa! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Nafasi ya Zungu hiyo, byuuuuuuuu! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Kashindwa! Kashindwa! Kashindwa! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI**: Mmeshindwa la kujibu. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Tumeona kwa hisani ya Rais. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI**: Kashindwa, kashindwa. *(Makofi/Kelele)*

**WABUNGE FULANI**: *Doctor! Doctor! Doctor! Doctor! (Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Amebebwa, amebewa! Amebebwa! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Unaweza Tulia unaweza! Kumbe wewe Tulia unaweza! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Amebebwa! Amebebwa! Amebebwa! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Ameletwa, uuh! Ameletwa uuh! *(Kelele)*

**SPIKA:** Naomba usikivu wenu!

**WABUNGE FULANI:** Amebebwa! Amebebwa! Amebebwa! *(Kelele)*

Mheshimiwa Sakaya ameshaingia eh! Ahsante sana, nafurahi tena kukuona. Eeh, huu mpambano wa akina mama mkali sana huu!

**MBUNGE FULANI:** Bora Zungu! *(Kicheko/Kelele)*

**SPIKA:** Inaonyesha wanawake wanaweza, au siyo jamani!

**MBUNGE FULANI:** Bora Zungu! *(Kicheko/Kelele)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwomba Katibu atupe kinachoendelea. Katibu! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Watu wote huku mmeonekana hamfai mpaka mkaletewa mtu! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Nyie wenyewe mmeletwa na mabwana zenu! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Kwani nyie mnafaa! *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Waache ku-*import* Wagombea. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Nyie wenyewe mmeimpotiwa. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Mnamwogopa ninyi! Mnamwogopa amewazidi kete! *(Kelele)*

**KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, naomba usikivu wenu! *(Kelele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa *Order, Order*, tumsikilize Katibu. *(Kelele)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, zoezi letu linalofuata ni kupiga kura. Naomba tuhesabiwe tena kwa sababu baada ya kupiga kura mara ya kwanza kuna baadhi yenu wametoka. Inatupa shida kuweka vizuri hesabu zetu. Kwa hiyo, naomba utulivu wenu na ikiwezekana milango ile ingefungwa ili tusihesabu kura mara mbili mbili. Naomba tuhesabu kura, tuhesabu idadi yenu. Tutazigawa kura na tutazikusanya.

Mheshimiwa Spika, naomba tufanye zoezi la kuhesabu.

**SPIKA:** Sasa Maofisa wangu fanyeni zoezi la kupata idadi ya Waheshimiwa Wabunge walioko ndani ya ukumbi huu ili tuweze kuendelea.

*(Hapa Maafisa wa Bunge walichukua idadi ya Waheshimiwa Wabunge waliomo Ukumbini)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Katibu tupatie idadi ya wapiga kura.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba radhi kidogo, kwamba Waheshimiwa mnapoingia na kutoka hesabu yetu inaharibika. Kwa hiyo, naomba tuvumiliane kwa muda mfupi tu kwa sababu zoezi lenyewe siyo refu.

Idadi ya Wabunge mliopo ndani kwa sasa ni 351. Nawaomba sana mwendelee kuwepo ndani ya ukumbi.

Pili, tunaamini kwamba kura yako ni ya siri, usimpe mtu kura yako. Tunaomba sana! Wakati wa zoezi la kukusanya tunasimama pembeni, mnazileta upande mmoja. Lakini ukipiga kura ukampa mwenzako, inaleta picha ambayo siyo nzuri kwamba kura hizi siyo za siri. Naomba Waheshimiwa Wabunge tulione hilo.

Mheshimiwa Spika, idadi yetu kikatiba ambao mpo sasa ni 369. *Quorum* ipo kwa maana ya akidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba tuendelee na zoezi. Naomba tuonyeshe masanduku ya kura.

*(Hapa Masanduku ya kura yalioneshwa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:**, ahsante.

Tunaomba Maafisa wenye kura mjongee mbele, kulia na kushoto, tunaomba mgawe kura kwenye makundi na Askari naomba msimamie. *Sargents*!

**SPIKA:** Naomba kura zigawanywe sasa, kila Mheshimiwa tupate kura moja moja. Kila anayepata kura apige katika jina mojawapo katika majina mawili ya Wagombea wetu.

Kama ilivyo ada, kama kuna Waheshimiwa ambao hawajapata kura, naomba wasimame ili irahisishe kuwafikia. Jamani, wahini eneo hilo hapo. Kila anayepata kura akae chini. Ukishapata karatasi yako unakaa.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani kila mmoja wetu ameshapata karatasi ya kura na ameshapiga kura.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Nadhani sasa Katibu, ni vizuri tukianza kuzikusanya kura zetu.

**T A A R I F A**

**MHE. MAULIDI S. A. MTULIA:** Taarifa Mheshimiwa Spika!

**SPIKA:** Ngoja tukusanye kura kwanza kidogo.

**MHE. MAULIDI S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, inahusiana na jambo hilo hilo!

**SPIKA:** Haya kaka. Kila anayesimama, ni lazima ajitambulishe kwa sababu bado ni wageni ili tuzoeane.

**MAULIDI S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naitwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni. Kuna wale wenzetu waliteuliwa hapa kama Mawakala kwenda kuhesabu kura za uthibitisho wa Mheshimiwa Waziri Mkuu mtarajiwa. Naomba wasisahaulike, wana haki ya kupiga kura.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu amekusikia. Naomba kura zikusanywe *chap chap!* Naomba Mheshimiwa Halima Mdee apewe kura, ndiyo ameingia sasa hivi. Naomba karatasi moja ya kura kwa Halima Mdee pale!

**MBUNGE FULANI:** Atulie kwanza!

**SPIKA:** Kuna Mheshimiwa yeyote ambaye kura yake haijakusanywa? Asimame pale alipo.

Kura zote zimekusanywa. Nawaomba mje basi Maofisa wangu. Tupate Wakala mmoja mmoja. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Wakala wako ni nani? Au unaamini meza?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA**: Mheshimiwa naomba nimchague Mheshimiwa Gekul akanisaidie kusimamia kura. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul tunakuomba hapa mbele. Mheshimiwa Tulia Ackson wakala wako ni nani?

**MHE. TULIA A. MWANSASU:** Mheshimiwa Spika, namteua Mheshimiwa Nape Nnauye kunihesabia kura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, naomba usogee hapa mbele.

Sasa naomba timu nzima iongozane iende kwenye chumba kilichoandaliwa na Katibu kwa ajili ya kuzihesabu kura hizi na kutuletea matokeo.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na kanuni, naongeza dakika thelathini ili tukamilishe zoezi lote hili; zoezi la Waziri Mkuu na zoezi la Naibu Spika ili jioni ya leo tuweze kufanya mambo mengine. Nadhani ni wazo zuri eeh? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sana!

**SPIKA:** Haya basi, tuwe na uvumilivu kidogo tunamaliza sasa hivi tu. Nisije nikasahau, nashindwa kutumia jina la Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu bado haijaundwa rasmi. Ndiyo nimewaandikia barua leo kwamba muunde Kambi Rasmi na mnitaarifu. Kwa hiyo, Upinzani mkutane Msekwa tutakapokuwa tumeahirisha baadaye. Mheshimiwa Mbatia amewaomba mkutane Msekwa.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, naomba tupokee matokeo ya kura ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi, Katibu wa Bunge.

Katibu wa Bunge naomba utusomee matokeo ya kazi yetu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nilete kwenu matokeo ya zoezi la upigaji kura ya kuthibitisha jina la Uteuzi wa Waziri Mkuu. Idadi ya Wabunge kikatiba ni 394, idadi ya Wabunge

waliosajiliwa ni 369, akidi ni 184, idadi ya Wabunge walioko ukumbini wakati wa zoezi la kupiga kura walikuwa 351, idadi ya kura zilizopigwa ni 351, kura mbili ziliharibika. Idadi ya kura halali ni 349.

Mheshimiwa Spika, Matokeo; idadi ya kura za "Hapana" ni 91, sawa na asilimia 25.9; idadi ya kura zilizoharibika mbili (2), sawa na asilimia 0.06; idadi ya kura za "Ndio" ni 258. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba nimalizie ili tuweke kumbukumbu sahihi. Kura 258 ni sawa na asilimia 73.5. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika naleta kwako ili uweze kumtangaza Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa matokeo hayo, napenda kulitangazia Bunge hili na kuwatangazia Watanzania kwa ujumla kwamba uteuzi wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, umepitishwa na Bunge hili, ili Mheshimiwa Majaliwa aapishwe kuwa Waziri Mkuu kwa asilimia 73.5. *(Makofi/Vigelegele)*

Katika nyakati hizi ushindi huu ni ushindi huu ni ushindi wa kimbunga! Ni ushindi mkubwa sana! *(Makofi)*

Napenda kuchukua nafasi hii binafsi kumpongeza sana Mheshimiwa Majaliwa, lakini kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza sana Mbunge mwenzetu huyu kwa imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais Magufuli ameionesha kwake. Ni mtu muhimu sana ambaye tutamhitaji katika kazi zetu kama Kiongozi wa shughuli za Serikali humu Bungeni.

Mimi binafsi nimhakikishie kama Spika wa Bunge hili nitatoa kila aina ya ushirikiano kwake na kwa Mawaziri wenzake. Naomba vivyo hivyo Waheshimiwa Wabunge wote tumpe ushirikiano tuweze kufanya kazi kwa pamoja kwa ushirikiano mkubwa ili tuweze kuwahudumia Watanzania wetu kama inavyotarajiwa. *(Makofi)*

Maelekezo mengine yatatoka kuhusu utaratibu mzima wa uapishwaji wake ambao huenda ukawa kesho, lakini maelezo yatatoka baadaye na maandalizi yatafanyika. Kwa kuwa uapishwaji utafanyika Chamwino Ikulu, kutakuwa na usafiri ambao umeandaliwa kwa ajili ya Wabunge wote, mawasiliano mtapata kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge. Nitawaomba wote tujiandae kwa ajili ya zoezi hilo muhimu. Ni vizuri kushiriki mambo haya makubwa ya Kitaifa na hasa sisi kama Wabunge na tutakuwa na nafasi za kukaa ambazo tumewekewa sisi kama Wabunge. Kwa hiyo, ni vizuri kufika mapema ili tuweze kushuhudia zoezi hilo likifanyika hiyo kesho.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa rasmi kama nilivyosema, tutawaleteeni baadaye. Cha muhimu ni kwamba sisi kama Bunge tumeshamaliza kutekeleza wajibu wetu wa Kikatiba wa kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, sasa tunaye Waziri Mkuu Mteule hadi atakapoapishwa hapo kesho ili kuwa Waziri Mkuu kamili.

Waheshimiwa Wabunge, tusubiri kidogo tu, tutapata matokeo mengine, haitachukua muda mrefu hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Majaliwa kama yupo karibu, nadhani ni vizuri nikamwita ili aje apate nafasi ya kuzungumza na sisi kwa dakika chache kidogo, apate nafasi ya kushukuru.

Mheshimiwa Majaliwa karibu sana hapa mbele. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walimwimbia Mheshimiwa Majaliwa Tuna imani na Majaliwa! Oyaa, oyaa, oyaah! Majaliwa Kweli; Kweli! Kweli; Kweli kweli kweli Majaliwa! Majaliwa kweli, kweli; kweli, kweli kweli kweli Majaliwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa na Waziri Mkuu Mteule; mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge ambao wamekupitisha kwa kura nyingi sana ili uweze kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia wao na Watanzania wote wanakusikiliza hivi sasa. Naomba nikupe dakika chache uweze kuzungumza na Wabunge hawa, lakini pia uzungumze na Watanzania. Karibu sana Mheshimiwa Majaliwa. *(Makofi)*

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA - WAZIRI MKUU MTEULE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia sisi wote kwanza kupita kwenye Majimbo yetu kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi ambazo zimetupa uhalali wa kuja kuwa Wabunge, kuwa Wawakilishi wao Watanzania wote ambao wameturidhia kuwa hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amemwongoza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kufanya kazi ya uteuzi wa jina langu. Jambo hili ni kubwa, sikulitegemea, lakini nimelipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kwa namna yeyote ile iliyomwongoza kulileta jina langu mbele ya Bunge lako Tukufu ikiwa ni pendekezo la uteuzi wa nafasi hii ya Uwaziri Mkuu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru wewe binafsi, lakini nianze pia kwa kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana zilizokupa mamlaka uliyonayo ya Uspika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chombo muhimu, mhimili muhimu na sote tulikuwa hapa, tulikupitisha kwa kura nyingi.

Pamoja na pongezi hizi, nakushukuru pia kwa kuendesha zoezi la leo la kupokea jina kutoka kwa Mheshimiwa Rais. Nilikuona nikiwa naangalia kwa njia ya Televisheni ulipokuwa unaendesha zoezi la ufunguzi wa bahasha zile zote tatu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa kuridhia na kulipigia kura nyingi jina langu ambalo limeletwa kwenu na Mheshimiwa ili muweze kuridhia tuweze kufanya kazi ya pamoja kwa Watanzania. Nawashukuru sana. Nataka niwahakikishie, pamoja na shukrani hizi kwamba nitawapa ushirikiano wa hali ya juu wote bila kujali Vyama vyenu. Ninyi wote ni Wawakilishi wa wananchi wa Tanzania, tutafanya kazi kwa pamoja ya ufuatiliaji wa shughuli zetu za maendeleo za kuisimamia Serikali yetu, nami nitasikiliza pia ushauri wenu katika kufanya kazi za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawafahamu vizuri wale ambao mnaendelea na Bunge hili, tumefanya kazi pamoja kwa miaka mitano iliyopita, tumeendelea kushirikiana, tumeendelea kushauriana na tumeendelea kufanya kazi kwa Watanzania wenzetu na bado niwahakikishie kwamba tutaendelea na wajibu ule ule wa kufanya kazi kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Taifa letu letu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuridhia jina langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru pia familia yangu ambayo imeweza kunivumilia wakati mwingi nikitekeleza majukumu yangu yaliyopelekea na ninyi kuwa na imani na mimi kupewa jukumu hili ambalo nitaanza nalo pindi nitakapoanza kupewa wajibu wangu. Vile vile nashukuru na nijenge imani kwao kwamba, wataendelea pia kunipa nafasi ya kufanya kazi za Watanzania nikishirikiana na ninyi pamoja. *(Makofi)*

Bila kuwasahau wapigakura wangu, wazee wangu, mama zangu, dada zangu na vijana wenzangu wa Ruangwa ambao waliridhia na mimi pia awamu hii ya pili kwangu kuwa Mbunge wao, kuwa mwakilishi wao, kuwa msemaji wao na kuridhia kuingia kwenye chombo hiki kikubwa na hatimaye leo kupata nafasi ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeunga mkono jitihada za wana Ruangwa nawashukuru sana Wana-Ruangwa kupitia chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawahakikishia Wana-Ruangwa kwamba tutaendelea kuwa pamoja kwenye shughuli zetu za kuijenga Ruangwa na bado wapate imani kwamba uwakilishi wao upo pale pale na tutaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watanzania wote kwa namna moja au nyingine, wako wengine walikuwa wananiombea dua wakati wote nipate maendeleo katika safari yangu ya maisha, lakini wapo ambao walikuwa wanapenda namna ambavyo nafanya kazi na wao kwa pamoja na hasa kwa jukumu ambalo nimelifanya kwa miaka mitano iliyopita, wanao mchango mkubwa wa msukumo wa mawazo ambayo pia yamemwongoza Mheshimiwa Rais kuweza kulichagua jina langu na kunipa jukumu ambalo amenipa. Nawashukuru sana Watanzania wote popote walipo.

Mheshimiwa Spika, nimepewa muda mfupi wa kusema neno, niseme kwamba sikuwa na maandalizi yeyote. Hata hiki kikaratasi nilichonacho hapa sijandika chochote! Hata hivyo, angalau imeniongoza kutambua uwepo wenu, mchango wenu mkubwa na bado nataka niwahakikishie wote kwamba kwa jukumu ambalo nimepewa, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kama Wawakilishi wa wananchi wetu, nitashirikiana na ninyi katika kufanya kazi zetu kwa Watanzania ambao wameridhia tuwawakilishe.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie nitafanya ziara kwenye maeneo yenu kuona changamoto zilizopo, kuona maendeleo mliyoyafikia, kuwasikia Watanzania wetu wana mawazo gani na sisi tufanye nini. Wakati wote nitakapokuwa nafanya jambo hilo, bado milango hiyo nitakayopewa itakuwa wazi kwenu wote kuja kutoa ushauri na yale yote ambayo mnayaona yanaweza kuleta tija kwa Watanzania.

Najua nitakuja kupata nafasi nyingine nzuri zaidi ya kuzungumza mengi, yale ambayo tutakuwa tumeyapanga vizuri ili mtoke mkijua jambo zima zuri ambalo tumelieleza. Kwa leo hii niendelee kuwashukuru na niwaombee pia maisha mema, Mwenyezi Mungu awape nguvu, awape uwezo, aimarishe busara kwetu, tuweze pia kujadili yale ambayo yatakuja mbele yetu kwa malengo ya kuleta maendeleo kwenye nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizi kwenu na ndiyo wajibu wangu mkubwa kwa siku hii ya leo, niseme tutaendelea kuwashukuru na kama ambavyo nimesema kuwapa ushirikiano, baada ya hapo tutapata nafasi nzuri ya kuzungumza na kubadilishana mawazo ya mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo yetu kwenye maeneo tunakotoka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Majaliwa *seat* yako, eeh, au bado kidogo! *(Kicheko)*

Ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu Mteule kwa hotuba yake nzuri sana kwetu wote Wabunge na kwa Jamhuri ya Muungano kwa ujumla wake.

Natumaini kila mwananchi amefurahi na kule Ruangwa sasa hivi hakukamatiki. Taarifa nilizonazo sasa hivi, shughuli kule ni kubwa! Wananchi wamefurahi sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kuvumilia kidogo ili Katibu amalizie kazi yetu ya zoezi la Unaibu Spika kwa sababu ni muhimu sana nipate msaidizi, maana hapa mbele bila kuwa na msaidizi patakuwa pachungu hapa!

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwamba kesho zoezi la Uapishwaji wa Waziri Mkuu linaanza saa 4.00 asubuhi Chamwino Ikulu na Awamu ya Tano ni awamu inayozingatia muda. Kule nafasi ya *parking* ya magari ni ndogo. Kwa hiyo, tumefanya mpango Waheshimiwa Wabunge mje na magari yenu myaache hapa, tutakuwa na mabasi maalum ambayo yatawapelekeni Chamwino wote kabisa. Kusafiri kwenye mabasi inafurahisha. Tunakuwa pamoja, tunazidi kufahamiana vizuri zaidi, tunatembea tuna-*chat* kidogo njiani.

Kwa hiyo, yatakuwepo mabasi yatakayowachukua Waheshimiwa Wabunge, mabasi hayo yanatondoka saa 2.00 juu ya alama hapa kwenye eneo letu la Bunge. Kwa hiyo, tuwahi mapema ili tuweze kuwahi kule Chamwino kwenye zoezi la uapishwaji wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba tukumbuke sana hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kama tunavyojua, tukitoka huko jioni ya kesho tuna kazi maalum hapa, natumaini kila Mheshimiwa Mbunge anafahamu kuhusu zoezi la kesho jioni.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu amesharudi. Naomba sasa tushirikiane katika kumsikiliza aweze kutusomea matokeo ya kazi yetu.

Katibu wa Bunge, nakukaribisha useme!

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nilete kwenu, Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya Uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Husikiki Katibu, tumia *microphone!*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena. Naomba nisome matokeo ya Uchaguzi wa Naibu Spika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge wote Kikatiba ni 394. Idadi ya Wabunge waliosajiliwa ni 369. Akidi ni 184. Idadi ya Wabunge waliopo Ukumbini na kupiga kura ni 351. Idadi ya kura zilizopigwa ni 351. Idadi ya kura zilizoharibika, hakuna.

Mheshimiwa Spika, matokeo; Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya amepata kura 101, sawa na 28.8%. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, amepata kura 250, sawa na 71.2%. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudisha kwako, ili uweze kumtangaza mshindi.

**SPIKA:** Kutokana na matokeo ambayo yamesomwa na Katibu wa Bunge hapa, naomba kuchukua fursa hii kumtangaza Mheshimiwa Tulia Ackson Mwansasu kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata 71.2% ya kura zote. Hongera sana Mheshimiwa! Hongera sana! *(Makofi)*

Ningechukua nafasi hii sasa, kwa sababu muda hauko upande wetu, nimpe Mheshimiwa Magdalena Sakaya dakika moja ya kushukuru halafu tuendelee na hatua nyingine.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maamuzi waliyofanya, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza mdogo wangu Dkt. Tulia kwa ushindi aliopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu na matarajio ya Watanzania kwamba chini ya uongozi wako ukisaidiana na Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa na Bunge imara, Bunge lenye kutekeleza wajibu wake kikamilifu, Bunge litakalofanya kazi zake tatu kwa ukamilifu wa hali ya juu; kazi ya Kutunga Sheria, Kazi ya Kuisimamia Serikali na Kazi ya Kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni tumaini langu na Watanzania kwamba, Bunge letu likiwa imara, likitenda haki, likifanya kazi kikamilifu, tutakuwa na Serikali iliyo imara. Serikali ikiwa imara itaweza kutekeleza wajibu wake vizuri kuhakikisha

kwamba Watanzania wanapata maendeleo, Watanzania wanapata imani na matarajio yao na imani yao inatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Mheshimiwa Tulia, dakika moja ya kushukuru! Hapo hapo ulipo!

**MHE. DKT. TULIA A. MWANSASU:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunifikisha hapa. Najua hii ni nafasi ya madaraka makubwa, lakini yeye amenifikisha hapa. Namshukuru sana na wote waliokuwa wakiniombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, pia nachukua fursa hii kumshukuru Rais kwa imani aliyoonesha kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru Wabunge kwa kura nyingi walizonipa kwa nafasi hii. Naahidi kwamba nitawatumikia mimi kama mtumishi wao, lakini pia nitashirikiana nao kwa kushirikiana na Spika kwa yale mambo yote ambayo Bunge linatakiwa kuyafanya kama kazi yake ya kuisimamia Serikali. Tutafanya kwa pamoja bila kujali tofauti za vyama ambavyo ndivyo vilivyotupa tiketi ya kuingia humu ndani. Nami naahidi kwamba tutakuwa pamoja na tutafanya kazi kwa ufanisi, nitatumia weledi wangu kusaidia Bunge hili, lakini pia kwa kushirikiana huko naamini mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, lakini pia naishukuru familia yangu kwa *support* yao kubwa ambapo wamenilea mpaka hapa nilipofikia. Vile vile namshukuru sana mume wangu kwa *support* aliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawaahidi Wabunge kwamba nitafanya nao kazi kwa unyenyekevu mkubwa, wasisite kuleta hoja zao kwangu nikikusaidia wewe katika kutekeleza majukumu yako.

Namshukuru sana pia Mheshimiwa Sakaya kwa Hotuba yake aliyoitoa na pia kwa changamoto aliyonipa, kwa sababu kama asingekuwepo maana yake pengine nisingepata fursa ya kujieleza. Nakushukuru sana Mheshimiwa Sakaya kwa kushiriki katika huu mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nami nachukua nafasi hii kama Spika, kumpongeza sana Mheshimiwa Tulia kwa kuchaguliwa kwake.

Namwahidi kabisa kwamba, tutafanya kazi kwa pamoja, kwa ukaribu mkubwa, *side by side* kuhakikisha kwamba tunasimamia na kutekeleza mambo yote ambayo tunatarajiwa kwayo na ninyi ambao tunawaongoza na kwamba Bunge hili la Kumi na Moja linakuwa ni Bunge bora zaidi kadiri inavyowezekana.

Kwa jinsi hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Tulia utapata kila aina ya ushirikiano kwangu na kwa kweli, ninavyoamini *you will enyoy* kuwa msaidizi wangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Baada ya hapo, sasa tunaingia katika utaratibu wa kumwapisha Naibu Spika. *(Makofi)*

**KIAPO CHA NAIBU SPIKA**

*(Hapa Mheshimiwa Dkt. Tulia A. Mwansasu aliapa Kiapo cha Unaibu Spika)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuruni sana kwa ushirikiano wenu kwa kazi hizi muhimu sana ambazo tumezifanya asubuhi ya leo na tumezikamilisha zote. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Tukumbuke kwamba kesho ni siku muhimu kama nilivyosema, kuna zoezi la Chamwino, lakini tunatakiwa tuwahi kurudi vilevile. Tuhakikishe kwamba kesho *by* saa 9.00 kila Mbunge awe ameshakaa hapa ndani kwa sababu kuna mambo mengi yatakayoendelea huko nje. Kuna shughuli nyingi, tuna wageni wengi sana kesho wa Kitaifa na Kimataifa. Kwa hiyo, nawaomba sana muwahi saa 9.00 Waheshimiwa Wabunge wote muwe mmekaa hapa ndani na utaratibu mwingine utaendelea kama utakavyokuwa umepangwa.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa 9.00 jioni.

*(Saa 7.37 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 20 Novemba, 2015 Saa 10.00 Jioni)*